https://dspace.org/

# Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto

**Matin, Ibrahim; Kisurulia, Simiyu**

**2021**
Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili
https://doi.org/10.37284/2707-3475
Matin, I., & Kisurulia, S. (2021). Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 3(1), 58-69.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 3, Issue 1, 2021**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto

*Ibrahim Matin[1] & Simiyu Kisurulia[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Rongo, S.L.P 103, Rongo, Kenya.
[2]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030, Kericho, Kenya
[*] Barua pepe ya mawasiliano: matinibrahim40@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*07 Juli 2021*

**Istilahi Muhimu**:

*Fasihi Ya Watoto, Nafasi, Tashbihi, Kufanikisha, Maudhui.*

**IKISIRI**

Makala haya yalichunguza jinsi wasanii wa vitabu vya fasihi ya watoto wamefuma tashbihi katika kazi zao ili kueleza maudhui yanayowalenga watoto kwa kuongozwa na nadharia ya umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure (1916). Kupitia kwa njia ya kiupekuzi na uchanganuzi matini, vitabu vya *Kisasi Hapana*, *Nimefufuka*, *Sitaki Iwe Siri*, na *Wema wa Mwana* viliteuliwa kimakusudi, vikasomwa na kuchanganuliwa. Tashbihi mbalimbali na maudhui ya familia, elimu, nidhamu, bidii, ugonjwa na kifo yalitambuliwa na kujadiliwa kwa undani. Uhusiano kati ya tashbihi na maudhui hayo ulidhihirishwa. Matokeo ya jinsi tashbihi zinavyofanikisha kueleza maudhui yaliwasilishwa kithamano. Utafiti huu umeonyesha tashbihi na maudhui katika kazi tulizohakiki na pia unachochea washikadau katika uwanda wa fasihi ya watoto kuhakiki kazi za watoto kabla kuwateulia kuzisoma.

**APA CITATION**

Matin, I. & Kisurulia, S. (2021). Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto. *East African Journal of Swahili Studies*, *3*(1), 58-69. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355.

**CHICAGO CITATION**

Ibrahim Matin & Simiyu Kisurulia. 2021. "Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto". *East African Journal of Swahili Studies* 3 (1), 58-69. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355.

**HARVARD CITATION**

Matin, I. and Kisurulia, S. (2021) "Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto", *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), pp. 58-69. doi: 10.37284/eajss.3.1.355.

**IEEE CITATION**

I. Matin, & S. Kisurulia, "Nafasi ya Tashbihi katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto", *EAJSS*, vol 3, no. 1, pp. 58-69, Jul. 2021.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**MLA CITATION**
Ibrahim Matin & Simiyu Kisurulia. "Halafu ya Sanaa za Ubunifu wa Kiafrika: Mtanziko Rejeleshi wa Tawala za Kiafrika". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 3, no. 1, Jul. 2021, pp. 58-69, doi:10.37284/eajss.3.1.355.

## UTANGULIZI

Watoto wanahitaji kuelekezwa tangu wanapozaliwa ili kuwa binadamu kamili wenye manufaa katika jamii. Katika kutimiza hili, washikadau hulazimika kutumia njia mbalimbali. Baadhi ya njia hizo ni matumizi ya fasihi ya watoto. Fasihi hii ina uwezo wa kutimiza hili kwa sababu elimu inahitaji mtu kutolewa katika lile analojua hadi lile asilojua ili kumsaidia kujenga tajriba yake maishani. Katika kutimiza hili tashbihi zinaweza kutumiwa kwa mafanikio makubwa kwa sababu zina uwezo wa kulinganisha mambo kwa kutumia yale anayojua mtoto ili kumsaidiia kuelewa yale asiyojua. Ingawa mwanzoni mtoto hughaniwa, kusimuliwa au kusomewa fasihi hii, baada ya muda huwa anaanza kujisomea na hili humsaidia kutalii ulimwengu wake na hivyo kujijengea tajriba yake mwenyewe.

Lengo la kutumia fasihi ya watoto katika kuwaelimisha limekuwa rahisi hasa kuanzia karne ya 18 kwa sababu hapo ndipo jamii ilianza kuona kuwa kazi za fasihi zinazowahusu watoto zijitegemee kwani hadhira hii ni ya kipekee (Bakize, 2014; Andrea, 2011).

Verma (2019) anakiri kuwa katika mwaka wa 2011 alipoanza kufanya uhakiki katika fasihi ya watoto, kulikuwa na waandishi wachache sana na vitabu vichache sana vilivyokuwa vimeandikwa kwa ajili ya watoto. Hata hivyo kumekuwa na mwamko mpya katika uwanda huu. Gatere (2020) akimnukuu Miricho na wenzake (2019) anahoji kuwa maendeleo ya fasihi ya watoto katika karne ya ishirini na moja yamepiga hatua kubwa kiasi cha kukiuka kanuni za fasihi hii kimaudhui kama zilivyowekwa na kuzoeleka katika kazi za miaka ya nyuma. Hili limechangiwa na sera na mifumo ya elimu kuhusu somo la Kiswahili nchini Kenya.

Licha ya kuwa vitabu vingi kuandikwa katika uwanda huu, Bakize na wenzake (2018) wanasema kuwa tafiti chache zimefanywa katika miongo miwili iliyopita na hii ni pamoja na Karuga (2005), Kairu (2005), Muthubi (2005), Mwanza (2007), Kavuria (2008), Ngugi (2009), Ruthiri (2012), Omuya (2017) na Akinyi (2017). Hata ingawa kunaweza kuwa na tafiti kadhaa za hivi karibuni, bado tahakiki zaidi kuhusu fasihi ya watoto zinahitajika kwa sababu waandishi wa fasihi wamejikuta wakiandika zaidi kuhusu fasihi ya watoto na vijana kwa sababu kumekuwa na mwamko wa usomaji sana kutokana na elimu wanayopata.

Baadhi ya tafiti zimefanywa zikilenga fani na maudhui. Hata hivyo kati ya tafiti tulizoweza kupitia, zilichunguza vipengele hivi katika upekee wake ambapo fani imechunguzwa kivyake na vilevile maudhui. Hata katika kazi zilizochunguza, vipengele hivi kwa pamoja hakuna kiliyoonyesha uhusiano uliopo kati yavyo. Hii ndiyo sababu uchunguzi wetu unapiga hatua katika kuendeleza tafiti za awali kwa kuchunguza jinsi vipengele vya fani vinavyofanikisha maudhui katika fasihi ya watoto.

Mbuthia na Miricho (2017) wanasema kuwa vitabu vya watoto vinapaswa kuhakikiwa kabla ya kuwachagulia wavisome kwa sababu vinaweza kuwaathiri watoto wasomaji kwa njia chanya au hasi kutegemea wamesoma nini. Walichokisoma kimesawiriwa kwa njia gani na kinasaidia kujenga uelewa na mitazamo gani kimaisha. Hii inamaanisha kuwa uhakiki wa kazi hizi una dhima ya kuzitathmini ili kutoa mwangaza na mwongozo wa kuziteua kwa watoto.

Ni kutokana na sababu hizi ambapo utafiti huu ulinuia kuchunguza namna fani inavyofanikisha maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunza fasihi katika shule za msingi nchini Kenya.

### Umuhimu na Sababu za Utafiti Huu

Kwanza kuhakiki fasihi ni kuikuza zaidi. Jambo la pili ni kuwa kumetokea waandishi wengi mahiri katika nyanja hii ya fasihi ya watoto na hivyo kuongeza haja wa kuzihakiki kazi hizi pindi zinapoandikwa ili kufuatilia maendeleo ya eneo hili katika fasihi ya Kiswahili. Mbuthia na Miricho (2017) wanakazia kuwa ipo haja ya kuchunguza mambo yanayowasilishwa kwa watoto kwa kuhakiki vitabu vya hadithi za watoto ili kubaini ni nini kinachosomwa nao, kama watoto wanasoma

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

mambo yanayofaa kwa ajili ya kuwajenga kimaadili na kuwapa mielekeo inayofaa ili jamii iwe na vizazi bora vya siku zijazo.

Kati ya tafiti chache tulizoweza kupata kuhusu fasihi ya watoto, hatukupata iliyochunguza jinsi tashbihi hutumiwa kwa utaalamu ili kufanikisha maudhui katika fasihi ya watoto. Kwa hivyo utafiti huu ulinuia kuweka bayana tashbihi mbalimbali zinavyochongwa na kutumiwa katika fasihi ya watoto kwa namna inayofanikisha maudhui katika kazi hizo mahususi. Tulichagua mada hii tukiwa na lengo la kutambua tashbihi na maudhui mahususi yanayopatikana katika fasihi ya watoto ili kung'amua kama yanafumbata hali halisi ya mahitaji katika jamii ya kisasa. Kazi hii tulitarajia iweze kutoa mchango katika kuhakiki fasihi ya watoto siku za usoni kwa kuonyesha waandishi na washikadau katika fasihi ya watoto maudhui na tashbihi mbalimbali katika vitabu tulivyohakiki. Kwa njia hii utafiti huu unatoa mchango katika kuboresha fasihi ya watoto.

## Misingi ya Nadharia

Nadharia ya umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa na jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi hiyo na vilevile namna sehemu mbalimbali za kazi za sanaa zilivyofungamana. Inazidi kushikilia kuwa sehemu hizo mbalimbali huweza kutenganishwa na kuchunguzwa na kuwa kazi yenyewe ilivyoundwa ndiyo hutoa maana. Yaani maana inayoibuliwa inavyoumbwa ina dhima kubwa kuliko maana yenyewe. Tulitumia mhimili huu kuchunguza madhumuni ya kwanza kwa kutambua tashbihi katika kazi tulizochunguza. Tulichukulia kuwa tashbihi kama kipengele cha fani ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii. Kwa kuongozwa na mawazo haya utafiti huu uliweza kutambua tashbihi mbalimbali katika riwaya zote nne na kisha kuzichunguza na kuzichanganua. Mhimili huu ulituongoza kuchunguza madhumuni ya pili katika utafiti wetu kwa kutambua na kutathmini maudhui. Tulichukulia kuwa kila maudhui ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii huku yale mawazo madogomadogo yanayochangia hayo maudhui makuu tuliyachukulia kama maudhui madogo.Kisha tukaonesha jinsi tashbihi hizo mbalimbali zimetumiwa kuendeleza maudhui tofautitofauti katika vitabu tulivyochunguza.

## MBINU ZA UTAFITI

Katika kuandaa makala haya, wandishi walifanya utafiti maktabani kwa kuchanganua matini kupitia kwa kusoma kwa undani vitabu tulivyoteua, magazeti, makala, tasnifu, nyaraka na taarifa mbalimbali maktabani na mtandaoni na hivyo tukapata habari za kina (Kothari, 2008). Idadi jumla ya utafiti wetu ilikuwa ni vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa katika kufundisha watoto walio katika shule za msingi nchini Kenya. Ingawa dadi kamili ya vitabu hivi haijulikani, kwa mujibu wa makala haya tulichunguza riwaya pekee kwa kuwa ilikuwa ni vigumu kutafiti vitabu vyote vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunza fasihi katika shule za msingi nchini Kenya. Tuliteua kimaksudi riwaya nne ambazo ni *Kisasi Hapana* (2008) iliyoandikwa na Ken Walibora, *Nimefufuka* (2011) iliyoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* (2008) iliyoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* (2012) iliyoandikwa na Nuhu Bakari. Mbinu hii ya uteuzi sampuli kimakusudi ilituwezesha kuteua sampuli iliyo bora, iliyo na data ya kutosha, iliyofaa utafiti wetu, tuliyoweza kumudu kiutafiti na ikatuwezesha kujibu maswali ya utafiti (Gall na wenziwe 1996).

Tulipata data kwa kusoma riwaya tulizoteua na kutambua data iliyooana na madhumuni ya makala haya kwa kudondoa maudhui na tashbihi mbalimbali na kuorodhesha. Tulichanganua tashbihi ili kupata mikabala mbalimbali inamotumika kisha tulitoa ufafanuzi kuhusu jinsi tashbihi hizo vilivyofanikiwa kuchangiana ili kuleta maana iliyokusudiwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya umuundo na malengo ya makala haya. Tuliwasilisha data ya mwisho kithamano kwa kuzingatia maoni ya Truex (1996) ambaye anaeleza kuwa uchanganuzi matini kithamano humpa mtafiti nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele vya uumbaji wa sanaa na maana inayojitokeza katika vipengele hivyo. Katika muktadha huu vipengele vya uumbaji wa sanaa ni tashbihi ambazo zimechangiana ili kutokeza maana inayolengwa na waandishi ambayo ni maudhui mbalimbali.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

## MATOKEO

### Dhana ya Mtoto

Kulingana na Shirika la Leba Duniani (ILO), mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18. Maoni haya pia yanaendelezwa na (Bakize, 2014). Dhana ya mtoto inaweza pia kufafanuliwa kuwa binadamu ambaye ana umri wa miaka saba aanzapo masomo katika shule ya msingi na miaka kumi na mitatu anapobaleghe (Tucker, 1981). Kwa upande mwingine kulingana na shirika la UNICEF Kenya (2009), mtoto katika shule za msingi nchini Kenya anapaswa kuwa kati ya miaka 6 na 13.

Tulichukua msimamo kuwa mtoto ni binadamu kati ya miaka sita anapomaliza chekechea na kuingia shule ya msingi hadi miaka kumi na nane. Tunachukulia hivyo katika utafiti wetu kwa sababu tunachunguza fasihi ya watoto inayosomwa na watoto wa shule za msingi na ambao kwa kawaida huwa kati ya miaka sita na kumi na mitatu au angalau chini ya miaka 18.

### Maana ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto nisanaa maalum inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaowahusu watoto, hadhira yake ni watoto na ambayo msingi wake kidhamira huwarejelea watoto (Wamitila, 2003). Bakize (2014) na Miricho (2015) wanashirikisha watoto katika fasihi yao kwa kusema fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe na inahusu watu wa umri wa chini ya miaka 18. Fasihi hii huweza kujumuisha hadithi za watoto, visakale, vitabu vya picha simulizi vya watoto, vitabu vya vibonzo vyenye wahusika watoto na hata drama ambazo zimetungwa kwa ajili ya watoto wadogo na vijana.

Kwa hivyo sisi katika utafiti wetu tulichukulia fasihi ya watoto kuwa ni sanaa itumiayo lugha sahili kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo na umri wa kati ya miaka 6 na 18.

### Dhana ya Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu viwili kwa njia waziwazi kwa matumizi ya viungio kama; mfano wa, mithili ya, sawa na, ja, kama vile na kadhalika (Wamitila, 2003; Msokile, 1992; Senkoro, 2011).Wamitila (2010) anaongezea kuwa tashbihiniulinganisho wa moja kwa moja na ulinganisho huo unadhamiriwa kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi.

Kulingana na Wamitila (2010) hakuna tashbihi hususa ambazo zimetengewa kundi fulani la wasomaji. Hata hivyo mwandishi huhitaji kuamua tashbihi zitakazotumiwa katika fasihi ya watoto kwakuongozwa na kaida fulani kwa sababu atataka kuwasiliana na msomaji wake vyema, kumshawishi na kumwathiri ipasavyo. Kwa hivyo nilazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kuwa ina uwezo wa kuwasilisha ujumbe huo. Kwa hivyo mbinu zinazotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa watoto huwazile zinazowafaa kwa sababu mwandishi hulazimika kuziteua kimakusudi ili kuwafikishia ujumbe. Huck (2001) na Wambua (2001) wanaongezea kuwa mtindo anaotumia mwandishi lazima uwe na uwiano na hadithi yake katika upande wa ploti, maudhui, wahusika na mandhari. Pia tamathali za usemi ni lazima ziendane na umri wa watoto anaowaandikia. Tamathali hizo pia zinafaa zitumiwe kwa hadhari ili zisiwe nyingi kiasi cha kumfanya mtoto kutoelewa ujumbe. Mambo yanayoamua uteuzi wa tamathali ni kama vile umri, mapato, kiwango cha elimu cha walengwa, uana, imani na itikadi za jamii.Hii ina maana kuwa mwandishi wa fasihi ya watoto ana mipaka katika mbinu atakazotumia katika kazi yake. Anapaswa kutumia mbinu ambazo ni nyepesi, zinazoeleweka na zinazorejelea mambo yanayopatikana katika mazingira anamoishi mtoto anayelengwa (Bakize, 2014; Gituku , 1990).

Ni kutokana nasababu hizi ambapo utafiti huu ulinuia kutambua ni kwa njia gani waandishi wa fasihi ya watoto hutumia tashbihi zinazoeleza maudhui yanayowaafiki watoto.

### Maudhui katika Fasihi ya Watoto

Ntarangwi (2004) anasema kuwa maudhui ni kile kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi, yaliyomo au jumla ya mambo yote yanayozungumzwa katika kazi yoyote ya kifasihi na hujumuisha dhamira, falsafa, mtazamo, ujumbe, maadili, falsafa, itikadi na msimamo wa mwandishi. Maudhui huibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya kazi husika ya kifasihi (Wamitila, 2003; Wamitila 2002). Chimera na Kimani (1999) wanaongezea kuwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mawazo haya (maudhui) huweza kuwa ya kila aina kutegemea lengo la mwandishi na hadhira anayotaka kuifikia. Kwa sababu hii, mwandishi wa fasihi ya watoto anaposhughulikia maudhui katika kazi yake anapaswa kushughulikia masuala yanayoleta burudani kwa watoto, yanayowaletea manufaa na yenye azma kwao (Cass, 1967; Msokile 1992). Nao Syambo na Mazrui (1992) wanapendekeza maudhui katika kazi ya fasihi yawe ya kuonya, kutahadharisha, kukashifu, kuburudisha, kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo miongoni mwa mambo mengine. Maudhui tuliyotambua katika kazi tulizohakiki yameonyeshwa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali 1: Maudhui katika Fasihi ya Watoto**

| | Wema wa Mwana | Nimefufuka | Kisasi Hapana | Sitaki Iwe Siri |
|---|---|---|---|---|
| Familia | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Elimu | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Nidhamu | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bidii | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Nafasi ya jinsia ya kike | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Ugonjwa na Kifo | | ✓ | ✓ | ✓ |

Kutokana na data hii imebainika kuwa waandishi wote wanne wameangazia maudhui ya familia, elimu, nidhamu na bidii. Hata hivyo maudhui ya ugonjwa na kifo yametokezwa na waandishi wa *Nimefufuka*, *Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri*.

### *Tashbihi Zinavyoendeleza Maudhui ya Familia*

Tashbihi zimetumiwa na waandishi wote wanne katika kuendeleza maudhui ya familia. Riwaya ya *Kisasi Hapana* imetumia tashbihi tano kuendeleza maudhui ya familia. Kwa mfano:

> *Humwona (mama) kama, sijui niseme, mtoto mdogo au aliyefiwa.Kawaida kila nikimwangalia mama, machozi humtoka njia mbilimbili. Machozi humdondoka machoni kama chemchemi ya maji. Ilimradi tangu ulipoondoka nyumba yetu imefunikwa wingu la huzuni.Majonzi.Simanzi tele* (Uk. 1).

Katika tashbihi hii "humwona mama kama aliyefiwa" mwandishi Ken Walibora ameangazia maudhui ya familia kwa kutuchorea familia ya Andrea Mukulu ambaye alikuwa anafanya kazi ya bawabu mjini. Mukulu aliishia kufungwa jela akiwaacha washiriki wa familia wengine kama mama yake, mke wake na watoto wakiteswa na majonzi ya kumkosa mpenzi wao. Mtoto wake Kido katika barua yake kwa babake anatumia tashbihi hii kuonyesha majonzi anayopitia mamake ambaye ni mke wa Mukulu. Mama huyu anashinda akilia kwa kumkosa mumewe. Kwa kutumia tashbihi "machozi humdondoka machoni kama chemchemi ya maji" mwandishi anatuonyesha hisia za Kido pamoja na mamake kuwa wana majonzi kiasi cha kutokwa na machozi kama chemchemi ya maji. Kiasi cha machozi kimetiwa chumvi ili kuonyesha kulia kupita kiasi kwa sababu ya hisia nzito za mama huyu kuelekea mwenzi wake katika familia ambaye ametiwa mbaroni. Kido pia hulia kila mara mamake anapolia. Ni kweli kuwa Kido hajui kwa nini mamake analia lakini bado yeye hulia tu. Hii ni ishara tosha kuwa katika familia hii washiriki wanajali hisia za wenzao.

Tashbihi pia inatumiwa kudhihirisha kina cha uhusiano kati ya Kido na nyanyake. Mwandishi kupitia kwa Kido anasema:

> *Baba mimi nilimpenda nyanya sana. Naye alinipenda kama mboni ya jicho.*
>
> *Eeh! Nyanya alinipenda kwelikweli* (Uk. 2).

Mboni ya jicho ni sehemu iliyo katikati mwa jicho na hupendwa na kutunzwa ili isiguswe na chochote kwa sababu ndiyo hutumiwa kuona. Jicho pia ni taa ya mwili mzima. Kusema kuwa nyanya alimpenda na kumtunza mjukuu wake Kido kama mboni ya jicho lake ni ishara tosha kuwa mapenzi kati yao yalikuwa ya kina na nyanya alimwona Kido kama taa na tegemeo katika jamii hii kwa sababu alikuwa ni mwanamume pekee aliyebaki baada ya babake kufungwa.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

Tashbihi tatu zimetumiwa katika kuendeleza maudhui ya familia katika *Sitaki Iwe Siri*. Kwa mfano mwandishi anatumia tashbihi kuhusu jicho akimrejelea Mwalongo kwa kusema:

> *"Aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho"* (Uk. 10).

Hili linamaanisha kuwa Mwalongo aliwakimu wajukuu wake kwa hali na mali. Tunaambiwa kuwa aliwaandalia kiamsha kinywa asubuhi na mapema kabla hawajaenda shuleni na kula chajio pamoja. Ili kutimiza mahitaji haya nyanya Mwalongo alifanya kazi za kilimo na ufugaji.

Katika *Wema wa Mwana* sababu za Kido kumpenda nyanyake pia zinaonyeshwa kwa kutumia tashbihi. Kido anasema:

> *"Nyanya alikuwa mpishi bora. Mpishi bora kama mama. La, mpishi bora kuliko mama"* (Uk. 2).

Watoto wadogo hupenda mama zao kuliko mtu mwingine yeyote kwa sababu mama ndiye huwa nao pindi nyingi na ndiye huwatimizia mahitaji yote ya kimsingi kama vile kuwaandalia chakula. Kwa hivyo kulinganisha mapenzi ya nyanyake na ya mama inamaanisha alimpenda kwa moyo wote. Jambo la pili lililomfanya Kido kumpenda nyanya yake ni hadithi zake ambazo Kido anakiri kuwa zilimfunza na kumburudisha. Anatumia tashbihi nyingine kuonyesha jinsi alivyothamini sana hadithi hizi. Anasema:

> *"Alitamba (nyanya) huku anaimba beti za mashairi na kuimba nyimbo kwa sauti nzuri kama ya ninga"* (Uk. 3)

Hapa Kido analinganisha sauti ya nyanyake na ya ninga kumaanisha aliithamini sana sauti hii. Watoto wa kiume hupenda kuwinda sana ndege lakini si ajabu kupata watoto wakimsikiliza ninga akiimba badala ya kumuua. Sababu ni kuwa wanapendezwa na sauti zao tamu. Kwa hivyo kupitia kwa tashbihi hii tunagundua kwamba daraka muhimu la familia ni kupitisha turathi muhimu kwa watoto kwani katika familia nyingi za Kiafrika hili linapitishwa kwa njia ya hadithi. Mwandishi anaonyesha kuwa Kido anatambua hili kupitia kwa maneno yake anayoyasema kwa kutumia tashbihi:

> *"Lakini kilichonifanya nimpende zaidi ni ngano alizonitambia. Ngano zake ziliniburudisha, zikanifunza na kuniliwaza. Zilinipa sababu ya kuishi. Zilikuwa tamu kama chakula chake"* (Uk. 3).

Hadithi hizi anazotaja alitambiwa wakila na hili linaonyesha uhusiano mzuri wa familia hii. Nyanya alitumia hadithi hizi kufunza mjukuu wake maadili mema.

Katika *Sitaki Iwe Siri*Mwalongo anawatunza wajukuu wake kihisia moyo na hili ni jukumu la washiriki wa familia. Mwandishi anasema kuwa walikuwa na mazungumzo kila jioni baada ya shughuli za siku. Katika pindi kama hizi aliwafunza mengi nao pia wakaulizia mengi. Tunaambiwa:

> *"Je mbona wajukuu hawa wana maswali mengi kama chiriku"* (Uk. 5).

Hili ni dhihirisho tosha kuwa watoto huwa na maswali mengi ili waelewe ulimwengu wao. Wanataka kuelewa vizuri mambo wasiyojua.Hata hivyo Nyanya Mwalongo alihofu kuwa kupitia kwa maswali haya siku moja wangemuuliza kilichoua wazazi wao kwa sababu hili lingemtonesha kidonda cha kuwapoteza wapendwa wake. Pia ni kama anahisi kuwa ni mapema mno kwa wana hawa kujua kilichsababisha kifo cha wazazi wao.Hili linaonyesha kuwa watoto wanapaswa kuelewa mambo hatua kwa hatua kadri umri wao unavyozidi kuongezeka.

### *Tashbihi Zinavyoendeleza Maudhui ya Elimu*

Kwanza kuna elimu ya wazazi kwa watoto wao ambayo iliendelezwa kupitia kwa hadithi walizohadithiwa jioni huku wakila. Kwa mfano katika *Kisasi Hapana* mwandishi anasema:

> *"Ngano zake ziliniburudisha, zikanifunza na kuniliwaza.Zilinipa sababu ya kuishi.Zilikuwa tamu kama chakula chake.Alitamba huku anaimba beti za mashairi na kuimba nyimbo kwa sauti nzuri kama ya ninga"*(Uku 3).

Pili kuna elimu ya shuleni.Katika elimu ya shuleni kuna sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ile ya kuendeleza vipawa vya wanafunzi na ya pili ni elimu ya vitabuni. Mwandishi ametumia tashbihi kuonyesha hisia za wanafunzi kulekea sehemu hizi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

mbili za elimu. Dada ya Kido anayeitwa Salama alikuwa msichana hodari sana darasani. Ndugu yake Kido anatumia tashbihi kwa kudhihirisha hili anaposema:

> *"Salama alikuwa mwanafunzi mzuri shuleni. Alifaulu kwenye masomo na michezo. Kama unakumbuka, Salama ni aina ya mwanafunzi ambaye kwake yeye kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala."* (Uk. 17)

Kwa kutumia tashbihi "kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala" Kido anakiri kuwa kuna wanafunzi wengine ambao ilikuwa rahisi sana kwao kupasi mitihani kama tu ilivyo rahisi kufumba macho kwani mtu hahitaji kutumia nguvu kufumba macho yake pindi anapohitaji kulala. Hata hivyo ni kawaida kwa wanafunzi kutofautiana katika viwango vyao vya elimu wanapokuwa shuleni kwa sababu hawawezi kuwa na uwezo sawa. Hili linaonekana katika maneno haya:

> *"Shule imeumbiwa watu kama Salama, sio watu kama mimi wasioweza kuunga moja na moja wakapata mbili"* (Uk. 17).

Mwanafunzi mwingine aliyekuwa na uwezo mkubwa darasani ni Samueli ambaye Kido anasema kumhusu kuwa, "Kwa hivyo niliwaachia mabingwa wa hesabu, kama akina Samueli, kuhesabu magoli".

Ni wazi kuwa wanafaunzi wengine wangefurahi sana ikiwa shuleni wangefunzwa tu michezo bila masomo ya darasa. Haya ndiyo matamanio ya Kido na yanaelezwa kwa kutumia tashbihi. Kido anasema:

> *"Kama shule ingekuwa mpira tu unachezwa, mbona ningependa shule kama mboni ya jicho langu? Ningependa shule kama ninavyopenda peremende na nyama ya kuku"* (Uk. 28).

Tashbihi hii "Ningependa shule kama ninavyopenda peremende na nyama ya kuku" inafaa kwa sababu watoto wanapenda vitu vitamu kama peremende. Hata hivyo kwao mchezo huzidi chakula hivi kwamba wao husihiwa tu wale iwapo chakula kitaandaliwa wanapocheza. Kwa hivyo wazazi na walimu lazima kwa kiasi fulani kukaza kamba ili kuwafanya watoto kuenda shuleni kwa sababu wao ndio wanaoelewa umuhimu wa elimu. Na hili hata watoto wenyewe wanajua kwa kuwa wanasema:

> *"Vinginevyo kwangu mimi shule ni kama dawa chungu ambayo mtu analazimishwa kumeza. Unameza tu maana wanaokupa wanadhani utafaidika, ingawa unaumia"* (Uk. 28).

Hapa Kido anaelewa kuwa dawa ni muhimu ili mtu aendelee kuishi lakini bado inabidi alazimishwe ndipo aweze kuimeza. Kwa jinsi hii pia watoto wengine hubidi walazimishwe ndipo waende shuleni kwa sababu walimu na wazazi ndio wanaojua umuhimu wa elimu kwa watoto hawa.

Kuhusu michezo, uwanja wao wa michezo na ubingwa wa Kido katika kandanda akiwa shuleni mwandishi anasema:

> *"Nikizifunga goli kwa urahisi kama kuteremsha maji kooni."*

> *"Wakati wa kiangazi (uwanja) una mavumbi kama jangwa na wakati wa masika au vuli una matope kama kinamasi"* (Uk. 22).

Kido anafafanua hali ya uwanja wao kwa kutumia tashbihi na hivyo kuonyesha hali ya uwanja huu pindi tofautitofauti katika mwaka. Hata hivyo jambo la msingi ni furaha yake kuelekea sehemu hii ya elimu anayoinea fahari hasa pale anapofunga wenzake magoli.

Shuleni wanafunzi hufundishwa na kuzoeshwa kufanya kazi chini ya usimamizi wa watu wengine. Hili linaonyeshwa kwa kutumia tashbihi Kido anaposema:

> *"Yaani pote (shuleni) hapo ni mahali ambapo maisha ya watu yanaendeshwa kama gari na watu wengine" (Uk. 13).*

> *"kaendesha gari kama vile walimu wanavyotuendesha sisi wanafunzi shuleni"* (Uk. 13).

Kwa mtoto gari huendeshwa kwa kasi na pia gari huwa halina hiari ya litakakoelekea. Ni juu ya dereva kuamua kasi na sehemu ya kwenda. Ndivyo ilivyo na wanafunzi shuleni. Hawana hiari ya la kufanya.Ni walimu wanaoamua.Na hili ndilo Kido hapendi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

Katika kuendeleza maudhui ya elimu,*Sitaki Iwe Siri* imetumia tashbihi kuonyesha namna wanafunzi wanavyobeba vitabu wanapoelekea shuleni:

> *"Walikuwa wamebeba mikoba ya vitabu vyao kama watalii"* (Uk. 12).

Wakati wa gwaride hasa wakati walimu walikuwa wanaongea mwandishi anasema hivi kuhusu kimya chao:

> *"(Wakati wa gwaride) mlio wa sindano sakafuni ungalitoa kishindo kikubwa kama cha bomu la atomiki"* (Uk. 15).

Katika tashbihi "kishindo kikubwa kama cha bomu la atomiki" maana inayojitokeza ni kuwa kimya kinaashiria kuwa elimu inahitaji utulivu na nidhamu na hilo ndilo linaonekana katika wanafunzi hawa.

Kupitia tashbihi tunagundua kuwa wanafunzi wenye bidii wakiwa shuleni muda wao huonekana mchache na huenda haraka sana kutokana na shughuli nyingi walizo nazo. Hubidi wanafunzi hawa kutenda kwa haraka na hili limeelezwa kwa kutumia tashbihi ambapo mwandishi anasema:

> *"Muda una mbawa kama ndege. Wakati wa Jumatatu hiyo ulionekana kukimbia sana"* (Uk. 22).

> *"Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia"* (Uk. 14).

Baada ya masomo ya siku wanafunzi walishangilia kwelikweli waliporuhusiwa kuenda nyumbani. Furaha yao inaonyeshwa kupitia kwa tashbihi:

> *"Alifululiza hadi eneo la paredi ambapo wanafunzi walikuwa wameanza kukusanyika huku wakipiga kelele kama bumba la nzi".* (Uk 58).

Shangilio hili linaashiria pumziko wanalopata baada ya siku yenye shughuli kwani elimu ni shughuli inayochosha akili.

Wakiwa shuleni wanafunzi bora hupewa kazi za ziada za kufanyia utafiti. Kwa mfano Musa anakubali kazi ya kufanya utafiti kuhusu Ukimwi ili hatimaye aandike insha itakayoshiriki katika shindano la kitaifa. Hii si kazi rahisi na mwandishi anaelezea daraka hili kwa tashbihi na kusema:

> *"Tangazo hilo la mwalimu mkuu lilimfanya ajihisi kwamba alikuwa amejitwika mzigo mzito kama nanga"* (Uku. 26).

Wanafunzi wanaopenda masomo yao hufurahia fursa wanazopata za kuendeleza kazi zao za ziada. Kwa mfano nyanya ya Musa anapompatia Musa ruhusa ya kwenda mjini ili kufanya utafiti, Musa anafurahi sana. Hisia zake zinaonyeshwa kupitia kwa tashbihi:

> *"Alifurahi kama kibogoyo aliyetunukiwa jino ombi lake lilipokubaliwa"* (Uk. 27).

***Tashbihi Zinavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu***

Mwandishi Bakari wa*Wema wa Mwana* ameliweka swala la nidhamu wazi kupitia kwa tashbihi anaposema:

> *"Nimechoka kabisa. Kesho napanga kumpeleka katika Shule ya Masomoni ya kurekebisha tabia.Huko atafunzwa adabu. Atanyooka kama mlingoti. Akirudi hapa nyumbani atakuwa na heshima zaidi"* (Uk. 13).

Kwa kutumia tashbihi "atanyooka kama mlingoti" tunaonyeshwa matokeo mema ambayo baba ya Ngoyoni anatarajia kuwa mwanawe atanyooka kama mlingoti ambao huwa ni mti unaotokana na mkonge na huwa haujikunji hata kidogo kumaanisha atakuwa amefunzwa nidhamu vizuri kwani yeye ameshindwa kumtia nidhamu pale nyumbani.

Watoto wanajua wanapokosa kuonyesha nidhamu.Hili linadhihirika wazi Mama Juma anapomkashifu Juma anapogundua kuwa ana tabia ya kuiba chakula kutoka jikoni badala ya kukaa na kusoma. Hili hata limeathiri matokeo yake katika mtihani. Anapogunduliwa mwandishi anatumia tashbihi kuonyesha mwitiko wa Juma. Anasema:

> *"Alishindwa kusema lolote.Uso ulimtuma. Macho yalilegea kama ya ndulele. Mwili ulilainika kama aliyezaliwa jana. Machozi yalimlengalenga asiwe na la kusema. ... Woga ulimvaa Juma mwili mzima.Wasiwasi ukampanda kwamba huenda baba*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

> *atamchapa. Alianza kutetemeka kama kuti la mnazi"* (Uk. 11).

Maana iyayojitokeza katika tashbihi "kulegea kama ndulele" na "kulainika kama aliyezaliwa jana" ni kutazama chini kwa aibu kuonyesha kuwa Juma alijua msimamo wa wazazi wake kuhusu uzembe shuleni na tabia yake mbaya ya kuiba chakula kutoka jikoni. Kuna uwezekano kuwa aliwahi kushauriwa kuhusu tabia hii. Kwa sababu kama hangejua ni kosa hangeaibika. Hii ndiyo sababu anatetemeka, kuogopa na kutokwa na machozi kwa kuwa alitarajia kupata adhabu kali na pia ni dhihirisho kuwa alijua amekosea. Tendo lake linaonyesha anatubu kwa kosa ambalo bila shaka alikuwa amekwisha kanywa alipokuwa anatiwa nidhamu.

Katika *Nimefufuka* ukosefu wa nidhamu unatokea pale ambapo Lena anamkosea mamake heshima alipoenda kumtafuta Mwambao. Alipompata alikuwa akifukuzana na wanaume. Mwandishi anadokeza sababu ya msichana huyu kujiona kuwa wa maana sana kiasi cha kukosa nidhamu. Mwandisi anatumia tashbihi mbili kudhihirisha hili. Anasema:

> *"Lena alikuwa mrembo kama malaika na hili likamfanya kuwa mwingi wa maringo kama tausi"* (Uku. 2).

Katika tashbihi hii tunapata kuwa Lena alikuwa mrembo wa kufananishwa na malaika ambao ni viumbe wa kimbingu wanaoaminiwa kuwa bila dosari yoyote kwa kuishi sehemu safi na hili lilimfanya kuwa na maringo makubwa. Urembo wake ulimfanya kupendwa na wanaume kila nui na hili likamfanya kuwa na kiburi na kukosa heshima kiasi cha kumpuuza mamake mzazi. Huu ni utovu mkubwa wa nidhamu. Kisha maringo yake yanafananishwa na ya tausi. Tausi ni ndege mwenye rangi za kupendeza na hutembea kwa madaha na kuonyesha rangi zake kwa kupanua mkia wake. Hili huonwa kama maringo na matembezi ya Lena yanafananishwa na tendo hili.

### *Tashbihi Zinavyoendeleza Maudhui ya Bidii*

Tashbihi zimetumiwa katika kuendeleza maudhui ya bidii katika *Sitaki Iwe Siri* ambapo tunampata Musa akiwa tayari kushiriki katika kuandika insha kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Mwandishi anamwonyesha Musa akijisemea na inaripotiwa kuwa:

> *"Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa. Alihisi msukumo wa aina fulani ukimchochea kushiriki kwenye shindano hilo… alijitia moyo kwamba lisilo budi hutendwa"* (Uk. 26).

Tashbihi hii "Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa" inamaanisha kuwa Musa alikuwa na wasiwasi kwa kiasi fulani kuingia katika kinyanganyiro hiki hata hivyo alijifunga kibwebwe na kuamua kujaribu kwa sababu alishakubali mbele ya mwalimu wake mkuu na hivyo akajitahidi ili ampendeze.

Pia tashbihi zinatumiwa kuhusu bidii katika shughuli za wafanyabiashara. Kwa mfano mwandishi anasema hivi:

> *"Kituo cha biashara cha Mwembe Tayari kilikuwa na shughuli nyingi kama za nyuki mzingani"* (Uk. 28).

Kuwa na "shughuli nyingi kama za nyuki mzingani" ni ishara kuwa kila mtu alikuwa ameshika kazi yake kwa bidii. Katika matatu inayowabeba Musa na dada zake kuna kondakta anayefanya kazi yake kwa bidii na tashbihi inatumiwa kudhihirisha hili:

> *"Utingo naye alikazana kama siafu kukusanya nauli kutoka kwa abiria"* (Uk. 29).

Mwandishi anaendelea kusema hivi kuhusu mkono wa kondakta:

> *"Mkono wake ulioonekana kukauka kama kibanzi cha ukuni"* (Uk. 30).

Hili ni dhihirisho kuwa utingo amefanya kazi hii kwa muda na kufanya mwili wake kukauka. Ni ishara ya bidii katika kazi hii. Kuhusu bidii ya madereva wamagari ya kubeba wagonjwa tunaambiwa hivi:

> *"Magari hayo yaliingia kwa kasi kama umeme kupitia lango kuu"* (Uk. 31).

Katika *Kisasi Hapana* Kido anahisi kuwa ile bidii aliyo nayo ni ishara ya nguvu na kuwa anaweza hata kuvunja miti ya simu ipitayo kwao kwa njia rahisi tu. Anasema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

> *"Nafikiri hata nikila nikashiba naweza kuzivunja kama kijiti kidogo au sio"* (Uk. 31).

Babake Kido naye anamtia Kido moyo ili atie bidii katika masomo jinsi anavyofanya katika mchezo wa kandanda. Anasema:

> *"Usichukie kusoma. Penda kusoma kama vile unavyopenda michezo. Kila kimojawapo ya vitu viwili hivi, kina umuhimu wake. Michezo inaweza kukupa sifa, labda pesa, kama zile wapatazo baadhi ya wanariadha na wanasoka wa kulipwa kutoka nchi kadha Barani Afrika"* (Uk. 37).

Hapa Mkulu analinganisha mapenzi ya Kido katika michezo na masomo na hivyo kumsihi mwana wake atie bidii masomoni pia na kwa kufanya hivi atafaidi kutokana na yote mawili.

***Tashbihi Zinavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo***

Hali ya afya ya Taabu mwana wa Lena katika kazi ya *Nimefufuka*aliyeachwa kutunzwa na Sikitu baada ya Lena aliyekuwa mamake kufa inaelezwa kwa tashbihi. Tunaambiwa:

> *"Mkojo nao kila siku ni kama mfereji usiofungika"* (Uk. 11).

Tashbihi hii "Mkojo nao kila siku ni kama mfereji usiofungika" inaonyesha namna ugonjwa ulivyomwathiri Taabu kwa kumfanya kulia kila mara na hili linamdhoofisha kiafya kiasi cha kushindwa hata kuthibiti mkojo wake. Picha tunayopata kutokana na tashbihi hii ni ile ya mtu aliyefungua mfereji wa maji usiosimama hadi anapoufunga tena. Kwa njia hii basi ni kama mtoto huyu anakojoa bila kusita na ni kama anasubiri mtu falani amfunge ndipo aache kukojoa. Hii ni chuku ya hali ya juu.

Pia kuhusu hali ya ya ugonjwa wa Jose mwandishi anasema:

> *"Jose ni msalaba mzito kama nanga"* (Uk. 13).

Hii tashbihi "Msalaba mzito kama nanga" inaonyesha hisia za Sikitu dada ya Jose kuelekea Jose. Jose amekuwa mlevi kiasi cha kumfanya kuwa mgonjwa na kuwa mzigo kwa wazazi wake na wengine waliokuwa na jukumu la kumtunza. Hawezi kujitunza kwa namna yoyote na hivyo kuwa mzigo unaobebwa tu kwa kujilazimisha kama nanga ilivyo mzigo mzito kwa meli ila hubebwa tu kwa kujilazimisha.

Mwandishi pia anatumia tashbihi kueleza kifo cha Lena kwa kusema:

> *"Ilikuwa mwiko mwana wao kuzikwa Mwambao kama mnyama asiye na wa kwao"* (Uk. 8).

Tashbihi hii inadokeza kuwa Lena aliugua na kisha kufa na sasa familia ya akina Lena walikuwa tayari kufanya yote yaliyokuwa katika uwezo wao ili kuleta mwili wa mwanao kutoka Mwambao ili azikwe nyumbani kwao.

Katika *Sitaki Iwe Siri* mwandishi anatumia tashbihi kueleza kuhusu hali ya afya ya watoto wa Mwalongo, Yusufu na Honorota hasa kabla ya kifo chao. Mwandishi anasema:

> *"Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani"* (Uk. 8)

Hili linamaanisha kuwa walidhoofika kupita kiasi kutokana na ugonjwa wa Ukimwikabla ya kifo kuwafika. Baada ya kifo chao tashbihi inatumiwa kuonyesha jakamoyo la Mwalongo mama yao:

> *"Mwalongo alikuwa ameganda kama kigaga pale nje na kuyakazia macho makaburi ya mwanawe na mkaza mwanawe"* (Uk. 9).

Kuganda kama kigaga ni tashbihi ambayo imetumiwa kuonyesha kuwa Mwalongo alikuwa amesimama mbele ya makaburi akiwa katika mawazo mazito yenye majonzi akifikiria wanae ambao walikuwa wamekufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi.

Kuhusu hali ya afya ya Mwalongo tunaambiwa:

> *"Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji na mgongo wake ulikuwa umepinda kama uta"* (Uk. 7).

Hii ni taswira iliyochorwa kwa mbinu ya tashbihi ya jinsi Mwalongo anavyoonekana. Hili limesababishwa na ugonjwa na hatimaye kifo cha wanawe ambacho kimeuatua moyo wake na kumpatia mawazo mengi yaliyoathiri afya yake.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

Mgongo unaweza kuwa umepinda kutokana nauzee au hata kazi nyingi za shamba akijaribu kupata mahitaji ya lazima ili kuwakimu wajukuu wake.

**HITIMISHO**

Imebainika katika utafiti huu kuwa kazi hizi zilizotungiwa watoto zimetumia tashbihi kwa kiwango kikubwa. Tashbihi hizi ni nyepesi na rahisi kueleweka na watoto kwani hazihitaji kufikiria mno. Zinatoa picha ya hali halisi maishani kwa urahisi katika akili ya walengwa. Ni rahisi kwa tashbihi hizi kueleweka na watoto kwani ni za moja kwa moja, zinahusu masuala yanayowahusu watoto, zinachota vilinganisho kutokana na mazingira halisi anayokumbana nayo mtoto kila siku akiwa nyumbani na shuleni, zinafanya mtoto kupata funzo mara moja na kumsaidia katika kumbukumbu na hivyo kumwelimisha na kumburudisha.

Pia imedhihirika wazi kutokana na utafiti wetu kuwa waandishi wote wanne walifanikiwa kujadili maudhui yanayoafiki watoto. Walijadili maudhui kama familia, elimu, nidhamu, bidii, ugonjwa na kifo. Maudhui haya ni maswala yanayohusu watoto kwa sababu mambo hayo ni mahangaiko yao makuu.Kwa ujumla basi waandishi hawa wamefaulu katika kusuka maudhui yao kwa kutumia kipengelecha tashbihi kwa njia mwafaka kwa hadhira lengwa.

**MAPENDEKEZO**

- Waandishi watiwe moyo kuandika zaidi kazi za watoto katika tanzu zote za fasihi.
- Waandishi watumie tashbihi zaidi katika kazi zao kwa sababu zinatoa ujumbe moja kwa moja na ni rahisi kueleweka.
- Kazi zilizoandikiwa watoto zihakikiwe kabla ya kuwateulia wazisome.
- Fasihi ya watoto ifanywe kuwa somo la lazima katika viwango vyote vya elimu kwa walimu ili wawe na uwezo wa kuifunza vema kwa manufaa ya watoto.
- Vitabu vya fasihi ya watoto vitumiwe na washikadau wote wa elimu ya watoto.

**MAREJELEO**


Andrea, A. (2011). *Social Issues in Contemporary African American Young Adult Ficton:* Iliyopakuliwa kutoka http://is.muni.cz/th/183848/pedf_m/social.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bakize, L. H., Ngugi, P. M. Y., & Lyimo, E. B. (2018). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto nchini Tanzania na Kenya: Mkabala Linganishi. *Kiswahili*, *80*(1).

Cass, J. E. (1967). *Literature and the Young Child*. London: Longman Group Ltd.

Chimera, R. & Kimani, N. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jommo Kenyatta Foundation.

Gall, D. M., Borg, R. W., na Gall, P. G. (1996). *Education Research: An introduction* (6thed.) New York: Longman Publishers.

Gatere, L. N. (2020). *Usawiri wa Familia ya Kisasa katika Fasihi ya Watoto Nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Gituku, N. (1990). *"Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Nchini Kenya*".Tasnifu ya M A, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Huck, C. (2001). *Childrens Literature in the Elementary School. 7th*ed. New York: McGraw-Hill Company.

ILO. (2017). *Global Estimates of Child Labour: Results and Trends, 2012-2016*. Geneva(…..)

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Miricho, M., & Mbuthia, E. M. (2017). The impact of the depiction of children in selected Swahili children stories. *International Journal of Contemporary Applied Sciences, 4*(1), 8-20.

Miricho, E. M. (2015). *Usawiri wa Watoto katika Hadithi za Mwepesi wa Kusahau na Likizo ya Mkosi.*Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.355

Miricho, M., Sheila, P. Wandera, S. na Nabea, W. (2019). *Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Mshikamano wa Kitaifa* katika Mwanga wa Lugha- Makala Teule ya Kongamano la Chakita 2018. Moi University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ntarangwi, M. (2004).*Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: IL 61201

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam. KAUTTU LTD.

Syambo, K. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Truex, D. (1996). Text-based analysis: A brief introduction. *College of Business Administration: Georgia State University*. *Retrieved on*, *10*(07), 05.

Tucker, N. (1981). *The Child and the Book.Apsychological and Literary Explanation.*Cambridge: Cambridge University College.

Verma, R. G (2019) Women Writers for Children in India: A Kaleidospic View. Sharma, V. (ed), *Feminist Discourses in Indian Context: Assertion, Identity and Agency*. New Delhi: Authorpress.

Wambua, M. S. (2001). *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo*. Tasnifu ya Uzimili, Kenyatta University.

Wamitila, K. W. (2010).*Kanzi ya Fasihi 1 Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Wide-Muwa.

Wamitila, K. W. (2003*). Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Toleo la Pili. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.